

Mkataba wa Kimataifa wa Bayoanuai

The Global Convention on Biodiversity (CBD)

Mkataba wa kimataifa wa Bayoanuai ya kibaiolojia ni nini?

Mkataba huu ni makubaliano ya nchi za dunia unaolenga ulinzi, uhifadhi na matumizi endelevu ya bayoanuai ya kibaiolojia pamoja na mgao sawa wa manufaa yake yatokanayo na rasilimali za kijenetiki.

Mkataba huu ulitiwa saini huko Rio de Janeiro, Brazil, mwaka 1992 na kuanza rasmi kutumika tarehe 29 mwezi Desemba mwaka 1993.

Misamiati muhimu:

(Biodiversity) Bayoanuai ya kibaiolojia - Hivi hujumuisha viumbe hai vikiwemo vya ardhini na majini.

Kongamano la vyama (Conference of parties) - Kongamano la vyama - hizi ni serikali za nchi zilizosaini mkataba huu wa bayoanuai. Wanachama hukutana kila baada ya miaka miwili.

Protokali (Protocols) - makubaliano madogo ndani ya Mkataba huu yanayohusisha masuala maalumu kwa nchi zinazojihusisha na masuala hayo ya bayoanuai. Protokali za mkataba ziko tatu, ambazo ni protokali ya Cartagena ya usalama wa bayoanuai na Protokali ya Nagoya ya mgao sawia na manufaa ya bayoanuai.

Malengo ya Aichi (The Aichi goals) - haya ni malengo ya makubaliano yatakayofikiwa na wanachama kupitia mkataba huu yaliyorasimishwa huko mjini Aichi nchini Japani mwaka 2010.

Mkataba wa Kimataifa wa Bayoanuai

The Global Convention on Biodiversity (CBD)

Tanzania na Mkataba

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni sehemu ya mkataba wa bayoanuai wa kimataifa. Kupitia mpango mkakati wa bayoanuai wa taiga, Tanzania inatekekeza makubaliano ya mkataba huu kwa njia zifuatazo:

- Kujumuisha masuala ya bayoanuai kwenye mikakati ya kitaifa ya maendeleo, mipango na bajeti za serikali za mitaa.
- Kujenga uwezo na kufanya kazi pamoja na taasisi za sekta mbalimbali juu ya bayoanuai.
- Kuelekeza rasilimali fedha kwenye miradi jengefu na stahimilivu juu ya bayoanuai.
- Kueneza uelewa mpana zaidi juu ya masuala ya bayoanuai kwenye jamii.

Wito kwa Vijana

- Kujifunza juu ya Mkataba wa kimataifa wa bayoanuai, mpango mkakati wa taifa wa bayoanuai na sera nyingine na kisha kuwasambazia watu wengine.
- Kuvumbua masuluhisho na miradi endelevu juu ya changamoto za bayoanuai kwenye jamii zetu.
- Kujihusisha kwenye majadiliano juu ya bayoanuai kuanzia ngazi ya familia hadi ya Mkataba huu wa kimataifa.

Nikupashe!

- Tarehe 22 Mei ndio siku ya Kimataifa kwa Mazingira Yenye Viumbe Hai (International Day on Biodiversity).
- Tanzania inabeba sehemu za Kimkakati sita (6) za bayoanuai ulimwenguni kati ya ishirini (20) zilizopo.
- Msimamzi wa Tanzania ni Mr. Faraja Ngerageza (ngerageza2001@yahoo.co.uk)



Katibu Mtendaji wa Sekretarieti ya Mkataba wa Kimataifa wa Bayoanuai ya kibaiolojia, (CBD) wa sasa ni mtanzania aitwaye Bi. Elizabeth Maruma Mrema



Convention on
Biological Diversity



Prepared by Careen Joel Mwakitalu

AWF/UNEP Policy Fellow